

**Dondoo za mukutano wa umma wa wapanda balskeli Dar es Salaam**  
**Tarehe 1 Julai 2006**

**Waliohudhuria**

Athman Kaya

Elaine Baker

Juma Ali Jongo

Shukuru Hassan

Ripoti ilitolewa kwenye mukutano kati ya TANROAD na UWABA wa tarehe 24 Mei. Zaidi ya wanachama 10 wa UWABA walihudhuria na zaidi ya wawakilishi 5 wa TANROAD Dar es Salaam walikuwepo. Mada ilitolewa na mejah akisaidiwa na wanachama iliyohusisha picha kwenye kuta (projekta).

Baada ya mukutano, Elaine aliandika barua ya kufuatilia TANROAD kuomba maelezo zaidi waliyoahidi ikiwemo orodha ya barabara zilizo chini ya uangalizi wao. Na ratiba zao za mahojiano.

Elaine pia aliandika barua tatu kwenda wilaya za ilala kinondoni na Temeke. Barua hizo ziliomba orodha ya washauri na pia UWABA iliomba kukutana na wawakilishi wa baraza. Temeke ilijibu na kuambatanisha orodha.

Elaine aliandaa vitambulisho vya UWABA kwa kutumia nembo iliyotengenezwa na meja. Walitumia picha za “digital” kuchapa. Mwanachama yeoyote atakayehitaji kitambulisho afuate Elaine au meja ili kupigwa picha vitambulisho vya Juma na Elaine vilikuwa tayari.

Juma aliarifu kuwa CHABADA chama cha balskeli Dar es Salaam – kikundi shindani cha wapanda balskeli kitakuwa na mashindano tarehe 7 julai. Wanakutana kila jumatatu kwa mazoezi.

Juma aliarifua pia kwamba Upendo Disabled Sports Club imewaalika wawakilishi wa uwaba kwenye mukutano tarehe 2 Julai.

Eline aliarifu mwendo kwenye tovuti na kuomba majibu kutoka kwa wale wenye kuweza kutumia mtandao wa internet. Othman alikubali kuandalia sehemu na kufanya mamuzi

Ilikubalika kuwa tuandae mukutano na halmashauri za manispaa kwa kuchunguza barabara ndogo chini ya wajibu wao. Ilikubalika kuwa tufanye hivi kwa makundi kundi la kwanza litakwenda Temeke tutakutana uwanja wa taifa saa 2 asubuhi siku ya jumamosi tarehe 8 au 15 kulinga na upatikanaji wa kamera za “digital” juma alisema atafuatili aTANROADS kuhusu orodha ya barabara zilizo chini ya uangalizi wao ili kupata orodha ya barabara zilizo chini ya manispaa. Elaine alikubali kuwasiliana na wanachama wa UWABA waishio Temeke kuwashawishi kushiriki.